JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI.

**NAMBA ZA SIMU**
MKUU WA SHULE 0754837625/0756241688
MAKAMU /MKUU WA SHULE 0764109889
PATRONI 0769274927

SHULE YA SEKONDARI PUMA,
S.L.P 429,
SINGIDA,

MZAZI/MLEZI WA ............................................
.........................................................................
S.L.P...............................................................

YAH.MAELEKEZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YZA SEKONDARI PUMA ILIYOPO HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI MKOA WA SINGIDA MWAKA……………….

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga kidato cha tano katika shule hii mwaka…………… na atasoma tahasusi ya HKL.

Shule ya sekondari puma ipo umbali wa kilometa 1 mashariki mwa mji wa puma na kuwa usafiri wa pikipiki wa tshs 2000/ hadi shule ilipo.

Usafiri wa hiace /noah kutoka mjini singida unapatikana katika kituo cha mabasi /stendi ya vumbi nauli tshs 3000/ kwa wale wanaotokea mikoa ya Manyara, Arusha, Tanga, Moshi lakini kwa wale wanaotokea barabara ya DAR ES SALAAM kwa mikoa ya Dodoma, Morogoro, Iringa, Mbeya, Katavi, Songea, Ruvuma watashukia stendi ya Puma kabla ya kufika singida mjini.

Kwa barabara kuu inayotoka MWANZA KWENDA DAR ES SALAAM kwa mikoa ya Shinyanga, Kagera, Kigoma, Geita, Mwanza, Simiyu, Mara, Tabora watashukia stendi ya Puma kilometa 16 baada ya kupita singida mjini.

THE HEADMASTER
PUMA SECONDARY SCHOOL

Muhula wa Masomo unaanza tarehe itakayotangazwa na Serikali. Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kutokana na tangazo hilo.

**1. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**1.1 Sare za Shule**

i. Sare yashule hii ni kitambaa chenye Rangi ya Darkbluu. Suruali mbili, marinda mawili.
ii. Mashati mawili meupe ya mikono mirefu
iii. Sare ya Michezo ni bukta 2 za rangi ya bluu,raba pea2
iv. Viatuvya shuleni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
v. Soksi jozi mbili nyeupe/nyeusi/khaki za shule;
vi. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali;
vii. Sweta 2 za rangi ya kijivu.
viii. Nguo za kushindia(*shambadress*)(***suruali mbili rangi nyeusi yenye marinda mawili na track suit rangi ya blue bahari na tisheti ya damu ya mzee***);
ix. Tai ndefu ya rangi ya darkbluu
x. Bima ya Afya uje nayo au unaweza kuja na ths 50,400/= kwa ajili ya kulipia bima ya Afya kwa mwaka mmoja
xi. Tisheti(T-shirt) *bluebahari(formsix),*

**1.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni: -**

i. Madaftari kauntaQ.4 ziwe saba
ii. **Ream(A4)**, Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika vya mtaala mpya, HISTORY, ENGLISH LANGUAGE, KISWAHILI, HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI NA ACADEMIC COMMUNICATION.
iv. File ya plastiki 1 kwa ajili ya kutunzia kumbukumbu za kitaaluma;
v. Godoro lenye upana wa 2.5 futi 6
vi. Mashuka Jozi 2ya rangi ya bluu bahari blanket1, chandarua 1rangi ya bluu, mto wenye foronya 1 ya rangi ya bluu
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula(sahani, bakuli,kijikonakikombe);
ix. Ndoo2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. Kwanja1, jembe1, reki1, mifagio 2 wa ndani na nje na sabuni ya maji lita 5

ANGALIZO: Mwanafunzi apangiwe kuleta kifaa kulingana na mazingira ya shule na tahasusi anayosoma

**1.1 Michango mbalimbali**

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha hizo za michango zilipwe kwenye akaunti namba 50806600060 yenye jina puma secondary school,bank ya NMB na mwanafunzi aje na pay in slip iliyoandikwa jina lake na mchanganuo wake**

2. **Sheria na Kanuni muhimu za Shule**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

**3.1 Sheria na Kanuni za Shule**

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa wanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2.Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

………………………………………………..

**HUSSEIN MTINDA MALONGA**

**MKUU WA SHULE**

*(Muhuri: HEADMASTER / PUMA SECONDARY SCHOOL / SINGIDA)*

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- Mkuu wa shule 0756241688
- Makamu Mkuu wa Shule 0764109889
- Mwandamizi Taaluma 0621241922
- Mwandamizi Malezi 0758315326

**PRIME MINISTER'S OFFICE**
**REGIONAL AUTHORITY AND LOCAL GOVERNMENT**
PUMA SECONDARY SCHOOL
P.O BOX 429 SINGIDA

**A: MEDICAL EXAMINATION FORM for Year** ...................................

4. To be completed by a medical officer in respect of all form I – VI entrants and new school employee
TO THE MEDICAL DOCTOR ................................... HOSPITAL/ HEALTH CENTRE BOX ...................................
Please Examine ................................... Age ................ Whether is fit to pursue studies/work ...................................
Test for
Blood (Red and white) ........................................................................
Stool examination ..............................................................................
Urinal ...............................................................................................
Syphilis ............................................................................................
Eye ..................................................................................................
Ear ..................................................................................................
Chest ...............................................................................................
Abdomen .........................................................................................
**B: ADDITIONAL INFORMATION:** Physical defects important, infection or family diseases act ..........................................................................................
**C:** I certify that the above-mentioned student is fit to pursue studies Medical Doctor's Signature ..........................................................................................
Name ........................................................................
Designation ................................................................
Station ......................................................................

THE HEADMASTER
SECONDARY SCHOOL
O BOX 429

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI PUMA S.L.P. 429 SINGIDA**
**FOMU YA KUKUBALI**

(Fomu hii pamoja na fomu ya afya na affidavit virudishwe shuleni siku ajapo mwanafunzi kuripoti)

MWANAFUNZI AJAZE SEHEMU HII

1. Mimi ........................................................... msichana/mvulana nimekubali kujiunga kidato cha ........................ shule ya sekondari Puma tarehe ..................................... nitafika shuleni bila kuchelewa. Nitatii sheria na nitaisihi maisha mazuri na nitakuwa mwanafunzi Mwenye bidii kwenye masomo na kazi za nje. Sitashiriki katika mgomo, fujo na Makosa ya jinai
2. Kama sitatimiza sheria na kanuni muhimu za shule hii naomba kuchukuliwa hatua za kinidhamu hii ni pamoja na kufukuzwa shule kwa makosa yasiyovumilika.

MZAZI/MLEZI AJAZE SEHEMU

1. Mimi ............................................................................ Nimekubali mtoto wangu (Jina) ............................................................... Asome katika shule ya sekondari Puma kuanzia .................................. naahidi kumpatia vitu vyote vinavyotakiwa kufika navyo shuleni kama ilivyotajwa katika barua ya masharti ya kujiunga na shule.
2. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria zote za shule nakuishi maisha mazuri na kuwa na bidii kwenye masomo na kazi. Nakiri nitalipa michango iliyoainishwa na sitaleta usumbufu kwa mwanangu na kwa uongozi wa shule.
3. Anwani yangu ya kudumu ni ...........................................................................................

Simu. ..........................................................

Sahiki ......................................................... Tarehe .......................................................

Wageni ninaowaidhinisha kumwona mtoto wangu awapo shuleni

i) ...................................................................... uhusiano wake ..................................

ii) ...................................................................... uhusiano wake ..................................

iii) ..................................................................... uhusiano wake ...................................

iv) ...................................................................... uhusiano wake ................................

THE HEADMASTER
SECONDARY SCHOOL
BOX 429